

# SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2 SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2 SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2

Friday 23 May 2003 (afternoon) Vendredi 23 mai 2003 (après-midi) Viernes 23 de mayo de 2003 (tarde)

#### 2 hours / 2 heures / 2 horas

## INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works, will not score high marks.

## INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.

#### INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

Andika insha juu ya moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei kwenye mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.

# Tamthilia

- **1**. *Ama* 
  - (a) "Hata kama tamthilia inajadili matatizo 'mazito' na 'nyeti', lazima iwe na sehemu ya 'ucheshi' ili kuondoa ukavu wa aina fulani." Katika kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, zingatia kwa kiasi gani na kwa jinsi gani matatizo mazito na nyeti yanavyosimuliwa yakiambatishwa na ucheshi.

Au

(b) "Katika tamthilia mwandishi inamlazimu kueleza kila kitu kupitia maneno ya wahusika wake." Kutokana na kusoma kwako angalau kazi mbili za sehemu hii, kwa kiasi gani unakubaliana na kauli hii na kwa kiasi gani unamchukulia mwandishi wa tamthilia kuwa uhuru wake wa kujieleza umefinywa?

#### Riwaya

- **2.** *Ama* 
  - (a) "Ploti au mpangilio wa matukio kiwakati na kimazingira ni jambo muhimu katika riwaya yoyote." Linganisha na kutofautisha ploti za angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

Au

(b) Katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, wajadili wahusika wakuu wawili kwa jinsi walivyochorwa na mwandishi, ukionyesha yupi anakuvutia na kujitambulisha naye kuliko mwingine.

#### Ushairi

- **3.** *Ama* 
  - (a) Kwa kutumia mashairi ya kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii onyesha matumizi ya picha na tamathali za semi jinsi zinavyoimarisha maudhui ya mashairi hayo.

Au

(b) "Kazi ya mshairi inatuvutia zaidi kwa vile ina nafasi ya uteuzi mpana wa mada na hisia mbalimbali." Kutokana na kazi angalau mbili ulizozisoma katika sehemu hii kwa kiasi gani unakubaliana na wazo hili.

# Riwaya ya Mapenzi

- **4.** *Ama* 
  - (a) Katika riwaya za mapenzi angalau mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, linganisha jinsi waandishi wanavyomtazama mwanamke kulingana na mwanamme.

Au

(b) "Katika riwaya ya mapenzi lugha husheheni 'chuku' na 'vitia chumvi." Kwa kurejelea kazi angalau mbili ulizozisoma jadili kwa kiasi gani unakubaliana na wazo hili.

# Masuala ya Ujumla

- **5.** *Ama* 
  - (a) "Kipengele cha usanii au umbuji ni kipengele muhimu sana katika kazi ya fasihi." Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutoka katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

Au

(b) "Si lazima wahusika katika kazi za fasihi wawe na uhalisia." Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutoka angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

Au

(c) "Kazi ya fasihi kila siku husawiri au kuakisi hali halisi ya jamii fulani." Je, unakubaliana na wazo hili? Jadili huku ukitoa mifano kutoka angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

Au

(d) "Mara nyingi katika fasihi wahusika wanawake huchorwa kama viumbe dhaifu na tegemezi kwa wanaume." Je, unakubaliana na wazo hili? Lijadili huku ukilitolea mifano kutokana na kazi angalau mbili ulizozisoma katika sehemu hii.